JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED

MWONGOZO WA USAJILI WA LAINI ZA SIMU KIBIOMETRIA

Umetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
Julai, 2019

Mwongozo wa Usajili wa Laini za Simu kwa njia ya Biometria katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

SEHEMU YA KWANZA
MAELEZO YA AWALI

1. Dondoo na tarehe ya kuanza kutumika

Mwongozo huu utajulikana kama *Mwongozo wa Usajili wa Laini za Simu kwa njia ya Biometria.*

2. Tafsiri ya maneno yaliyotumika

Maneno na istilahi kwenye Mwongozo huu yana maana zifuatazo:

" Mteja" ina maana ya mtu ambaye anapata, au anataka kupata huduma za aina yoyote kutoka kwa mtu anayeendesha shughuli kwa mujibu wa Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta za Usajii wa laini ikiwa ni pamoja na waliojiunga na huduma.

"Namba Tambulishi ya Laini", ambayo inajulikana Kama *Integrated Circuit Card Identifier* ina maana ya namba maalum ya utambulisho ambayo imechapwa na kuwekwa ndani ya laini ya mteja, na ni njia inayotumika kimataifa ya kutambua laini husika.

"EPOCA" ina maana ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Na. 3 ya mwaka 2010.

"IMEI" ni kifupisho cha *International Mobile Equipment Identity* na ina maana ya namba ya pekee ya kimataifa yenye tarakimu 15 ambayo inatumika kuitambua laini ya simu.

"IMSI" ni kifupisho cha *International Mobile Subscriber Identity*, na ina maana ya utambulisho wa kipekee unaotumiwa na watoa huduma za simu za mkononi kuwatambua wateja kwenye mitandao yao.

"Kifaa cha Mkononi" ina maana ya kifaa kinachotumika kwa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi ikijumuisha vifaa ambavyo vinaweza kupata tu huduma za data kwenye mitandao ya simu za mkononi.

"Kundi la Usajili wa kibiometria wa Laini za Taasisi" lina maana ya usajili wa Laini zitakatomiwa tu Taasisi.

"Kundi la Usajili wa Laini kibiometria kwa Mtu Binafsi" ina maana ya usajili wote wa laini kibiometria kwa matumizi tu ya mteja kwa matumizi yake binafsi.

"Kundi la Usajili wa Laini kibiometria kwa Mtoto" ina maana ya usajili wa laini kibiometria kwa ajili ya matumizi ya watoto tu.

"Kundi la Usajili wa Laini Kibiometria wa Raia wa kigeni" linajumuisha Usajili wa Laini zitakazotumiwa tu na raia wa nje.

"Kundi la Usajili wa Laini za Simu kwa kundi la Taasisi ya Kidiplomasia" ina maana ya usajili wa laini zote zitakazotumika tu na taasisi za Kidiplomasia.

"Kundi la Usajili wa Laini za Wanadiplomasia" linajumuisha usajili wote wa laini zitakazotumika tu na Wanadiplomasia.

"Kundi la usajiliwa Kampuni kibiometria" ina maana ya usajiliwa laini zinazotumiwa tu na Kampuni.

"Laini ya simu iliyo hai" ina maana ya laini ambayo inafanya kazi kwenye mtandao wa simu za mkononi.

"Laini ya Simu", ambayo pia inajulikana kama SIM Card ina maana ya kifaa cha kielektroniki kilichotengenezwa kutumika kwa mawasiliano kupitia simu za mkononi au vifaa vya mawasiliano, na ambacho kinawezesha watumiaji kuwasiliana.

"Laini za mkupuo" ina maana ya laini nyingi zilizosajiliwa wakati mmoja kwa ajili ya mawasiliano ya kielektroniki na ambazo zinahitaji kitambulisho cha NIDA na uhakiki wa kibiometria wa mwakilishi mmoja mbali na laini za ziada.

"Makundi ya Usajili wa Laini Kibiometria" ina maana makundi ya Kampuni, Mwanadiplomasia, Mtu Binafsi, Taasisi, Raia wa nchi nyingine, Mtoto na Wageni.

"Mamlaka" ina maana ya Mamlaka ya Mwasiliano Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya 2003.

"Mgeni" ina maana ya raia kigeni ambaye sio mwanadiplomasia na ambaye anakaa nchini kwa kipindi chini ya miezi sita (6).

"Mgogoro ambao haujapatiwa suluhu" ina maana ya mgogoro ambao hauwezi kutatuliwa na wahusika ndani ya muda uliowekwa kwenye kanuni hizi.

"Mkataba wa huduma" ina maana ya makubaliano yaloiyofikiwa kati ya mwenye leseni na mteja kwa ajili ya kutoa kwa mteja huduma zinazosimamiwa na leseni husika.

"Mlezi" ina maana ya mtu ambaye anawajibika na anamsimamia motto au mtu ambaye amekabidhiwa kwake kisheria, kupitia wosia au amri ya mahakama na kupewa kazi ya kumlea na kusimamia mali na haki za mtoto husika.

"MSISDN" ni kifupisho cha *Mobile Subscriber Integrated Services Digital Network* ina maana ya namba ya simu ambayo inamtambulisha kipekee mteja aliyejiunga na mtandao wa mtoa huduma.

"Mtoa Huduma" ina maana ya aliyepewa Leseni ya kutoa huduma za simu.

"Mtoto" ina maana ya mtu aliye chini ya miaka kumi na nane (18) na mwenye umti zaidi ya miaka kumi na mbili (12).

"Mtumiaji" ina maana ya mtu anayetumia mawasiliano ya kielektroniki au bidhaa au huduma za posta.

"Mwanadiplomasia" ina maana ya raia wa nchi nyingine ambaye yuko kwenye shughuli za kikazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambaye anatambuliwa kwa pasipoti ya kidiplomasia na kitambulisho cha kidiplomasia vinavyotumika.

"Mwenye Leseni" ina maana ya aliyepewa leseni na Mamlaka kutoa huduma na kufanikisha kutolewa kwa huduma za mawasiliano ya posta na kielektroniki, ambaye pia anajulikana kama mtoa huduma.

"Namba ya RB" ina maana ya namba kutoka kwenye daftari la kumbukumbu linalotumika kwenye utaratibu wa Jeshi la Polisi Tanzania, ikiwa ni pamoja na namba za rejea kwa laini za simu zilizoripotiwa kupotea, kuibwa au kuharibika.

"Raia wa Kigeni" ina maana ya raia wa nchi nyingine ambaye sio mwanadiplomasia anayeishi nchini kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita (6).

"Taasisi ya Kidiplomasia" lina maana ya taasisi ya kidiplomasia inayowakilisha taasisi ya kimataifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Taasisi" ina maana ya taasisi ya kiserikali au isiyo ya kiserikali ambayo inaendesha shughuli zake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Umoja wa GSMA" ina maana ya umoja unaojulikana kama Global System for Mobile Communications Association (GSMA) ambao ni umoja wa kimataifa wa watoa huduma za simu za mkononi kutumia mfumo wa tekinolojia ya GSM ambao lengo lake ni kuunga mkono, kuweka viwango, kueneza na kuhimiza matumizi ya mfumo wa simu za mkononi wa GSM.

"Usajili wa kibiometria wa Mgeni' ina maana ya usajili wa laini kibiometria kwa matumizi ya wageni tu.

"Waliojiunga kwa Huduma" ina maana ya mtu binafsi, kampuni au taasisi ambayo inapata au imejiunga na mtandao wa mtoa huduma za simu za mkononi.

3. Utangulizi

Mwongozo huu unaainisha utaratibu wa kusajili laini za simu kwa njia ya biometria. Unawahusu Watumiaji, Watoa Huduma na maeneo ya kibiashara yanayohusiana na usajili wa laini za simu.

4. Malengo ya Mwongozo wa Usajili wa laini za simu kwa njia ya Biometria

Yafuatayo ni malengo ya Mwongozo wa Usajili wa laini za simu kwa njia ya Biometria:-

(i) Kuhakikisha kwamba laini za simu za mkononi zinazohamishika, simu za mkononi zenye laini ndani au vifaa vya mawasiliano vyenye uwezo wa kutumia laini vinasajiliwa kikamilifu na taarifa zinawekwa sawasawa katika mfumo uliowekwa na Mamlaka.

(ii) Kuhakikisha kwamba wamiliki wa laini zote za simu za mkononi zinazohamishika, simu za mkononi zenye laini ndani au vifaa vya mawasiliano vyenye uwezo wa kutumia laini wanatambulika kiurahisi kwa kutumia utaratibu unaofaa wa utambulisho.

(iii) Kuimarisha na kuendeleza juhudi za kupambana na ulaghai katika miamala na huduma za kielektroniki.

(iv) Kuhakikisha kwamba watoa huduma wanakuwa na utaratibu unaofanana wa kusajili laini za simu kwa njia ya biometria.

SEHEMU YA PILI

WAJIBU NA MAJUKUMU

5. Wajibu

Wajibu wa wahusika katika usajili wa laini za simu kwa njia ya biometria ni kama ifuatavyo:-

a. Wajibu wa mteja wa huduma za simu za mkononi

(i) Kuhakikisha kwamba laini yake ya simu imesajiliwa kibiometria

(ii) Kuhakikisha kwamba ana Kitambulisho cha Taifa au Namba ya Kitambulisho cha Taifa au kitambulisho au namba kama itakavyoelekezwa na Mamlaka kabla ya kwenda kwa watoa huduma za simu za mkononi kusajili laini ya simu kwa njia ya biometria.

(iii) Kuhakikisha kwamba anahakiki usajili wa laini yake kwa kupiga namba *106#.

(iv) Kuhakikisha kwamba hatachangia na mtu mwingine yeyote namba maalum iliyoko kwenye laini yake ya simu.

(v) Kumtaarifu mtoa huduma yanapotokea mabadiliko ya mwakilishi wa kampuni husika na kumsadia mtoa huduma kumsajili mwakilishi mpya kwa mujibu wa sheria na kanuni au kwa mujibu wa Mwongozo huu.

(vi) Kumtaafitu mtoa huduma kuhusu mabadiliko ya mtumiaji au matumizi ya laini ya simu iliyo kwenye milki yake.

(vii) Kutoa taarifa Polisi au kupitia mfuko wa mtandaoni wa kutoa taarifa iwapo laini yake simu za mkononi inayohamishika, simu ya mkononi yenye laini ndani au vifaa vya mawasiliano vyenye uwezo wa kutumia laini vitapotea au kuibwa; ambako atatakiwa kupata taarifa za kupotea ndani ya simu saba za kupotea au kuibwa.

(viii) Kuwasilisha taarifa ya kupotea kwa laini ya simu kwa mtoa huduma wake anapoomba kupatiwa laini nyingine ya simu mbadala wa ile iliyopotea au kuibwa.

(ix) Kuitoa laini ya simu iliyoharibika kwa mtoa huduma kwa ajili ya kupatiwa nyingine.

b. Wajibu wa Watoa Huduma

(i) Kuhakikisha kwamba mfumo uliounganishwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) unafanya kazi wakati wote.

(ii) Kuhakikisha kwamba mfumo uliounganishwa kwenye kanzidata kuu ya usajili wa laini za simu iliyoko TCRA unafanya kazi wakati wote.

(iii) Kuhakikisha kwamba vifaa vya kufanya usajili wa laini za simu kwa njia ya biometria vimesambazwa kote nchini.

(iv) Kuhakikisha kwamba majina ya wanaosajiliwa na taarifa nyingine zinawekwa kama zilivyopatikana kutoka kanzidata ya NIDA.

(v) Kuhakikisha kwamba wateja ambao hawajasajiliwa kwa njia ya biometria wanapewa taarifa za tarehe ya mwisho ya usajili.

(vi) Kuzima laini zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa baada ya tarehe ya mwisho ya usajili.

(vii) Kuhakikisha kwamba vituo vya huduma kwa wateja, maduka au ofisi za wakala wa usajiliwa laini kwa njia ya biometria vinapatikana katika mikoa na wilaya zote.

(viii) Kuhakikisha kwamba laini za simu zinasajiliwa kwenye vituo vya huduma kwa wateja vilivyoidhinishwa; maduka ya watoa huduma au yale ya wakala yaliyoidhinishwa. Wakala wa usajili atatakiwa kupokea kitambulisho kinachokubalika au pasipoti zenye visa au pasipoti za wageni wasiohitaji visa.

(ix) Kuhakikisha kwamba laini za simu zinakuwa na namba za kuanzia na wateja wanaweza kuzibadilisha kuwa namba wanazozitaka wao kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta za usajili wa laini za simu za mwaka 2018 na marekebisho yake.

(x) Kuhakikisha kwamba taarifa za usajili ambazo zinaweza kuhakikiwa na NIDA zinawasilishwa kwenye kanzidata kuu ya usajili wa laini za simu iliyoko TCRA kadri zinavyopatikana.

(xi) Kubadilisha laini ya simu iliyoharibika baada ya kuhakiki usajili na umiliki wa awali kupitia uhakiki wa kibiometria.

(xii) Kuhakikisha kwamba laini zilizoharibika ambazo zinarudishwa zinahifadhiwa kwa kipindi kisichopungua miezi 12.

SEHEMU YA III

MWONGOZO

6. Utaratibu wa Kusajili laini zinazotumiwa na Watu Binafsi

(i) Laini zinazotumiwa na watu binafsi zitasajiliwa chini ya kipengele cha Usajili wa Kibiometria wa Mtu Binafsi.

(ii) Mteja atatakiwa kuwasilisha kitambulisho chake cha NIDA na alama za vidole kwa uhakiki kwa usajili wa laini ya simu.

(iii) Mtoa huduma atahifadhi kumbukumbu kwa mujibu wa ufafanuzi uliotolewa na NIDA.

(iv) Laini ya simu inayosajiliwa itakuwa na jina la mteja kama lilivyo kwenye kitambulisho cha Taifa.

7. Utaratibu wa Kusajili laini zinazotumiwa na Mashine au Vifaa vya Mawasiliano ya Kielektroniki.

(i) Mashine na vifaa vingine vya kawasiliano ya kielektroniki vitasajiliwa chini ya kipengele cha Kampuni.

(ii) Kampuni itatakiwa kuwasilisha nakala halisi zilizothibitishwa za Namba ya Mlipa Kodi (TIN), Leseni ya Biashara na Hati ya Usajili wa kampuni.

(iii) Mwakilishi wa kampuni atawasiliaha kitambulisho chake cha NIDA na uhakiki wa alama za vidole mara moja kwa kadi zaidi ya moja anayosajili kibiometria.

(iv) Mtoa huduma atatunza kumbukumbu za taarifa za kampuni na za mwakilishi wa kampuni husika.

(v) Laini itakayosajiliwa itakuwa na jina la Kampuni.

(vi) Pale ambapo mashine au vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinamilikiwa na watu binafsi, laini zitasajiliwa chini ya kipengele cha mtu binafsi kwa kutumia kitambulisho cha NIDA na uhakiki wa alama za vidole mara moja wa laini zote anazosajili kwa mara moja. Mtoa huduma atatunza kumbukumbu za mtumiaji binafsi na majina ambayo laini hizo zimesajiliwa; na jina la laini iliyosajiiwa litakuwa jina la mtu binafsi aliyefanya usajili.

8. Utaratibu wa kusajili Laini zinazotumwa na Wafanyakazi wa Kampuni

(i) Laini zinazotumiwa na wafanyakazi wa kampuni zitasajiliwa chini ya kipengele cha usajili wa laini za kampuni kibiometria.

(ii) Kampuni itatakiwa kuwasilisha nakala halisi zilizothibitishwa za Namba ya Mlipa Kodi (TIN), Leseni ya Biashara na Hati ya Usajili wa kampuni.

(iii) Kila mfanyakazi ambaye anastahili kutumia laini husika atatakiwa kuwasilisha kitambulisho chake cha NIDA na uhakiki wa alama za vidole kwa usajili wa laini kibiometria.

(iv) Mtoa huduma atatunza taarifa za kampuni na za wafanyakazi.

(v) Laini ya simu itakayosajiliwa itakuwa na jina la mfanyakazi husika.

9. Utaratibu wa kusajili laini zinazotumiwa na Kampuni

(i) Laini za simu zinazotumiwa na kampuni zitasajiliwa chini ya kipengele cha kampuni katika vituo vya huduma kwa wateja, maduka ya watoa huduma na ya wakala.

(ii) Kampuni itatakiwa kuwasilisha nakala halisi zilizothibitishwa za Namba ya Mlipa Kodi (TIN), Leseni ya Biashara na Hati ya Usajili wa kampuni.

(iii) Mwakilishi wa kampuni atawasiliaha kitambulisho chake cha NIDA na uhakiki wa alama za vidole mara moja kwa kadi zaidi ya moja anayosajili kibiometria.

(iv) Mtoa huduma atatunza taarifa za kampuni na za mwakilishi wa kampuni.

(v) Laini ya simu itakayosajiliwa itakuwa na jina la kampuni.

10. Utaratibu wa kusajili laini zinazotumiwa na Taasisi

(i) Laini za simu zinazotumiwa na kampuni zitasajiliwa chini ya kipengele cha Taasisi katika vituo vya huduma kwa wateja, maduka ya watoa huduma na ya wakala

(ii) Taasisi itatakiwa kuwasilisha barua ya utambulisho.

(iii) Mwakilishi wa taasisi atawasiliaha kitambulisho chake cha NIDA na uhakiki wa alama za vidole mara moja kwa kadi zaidi ya moja anayosajili kibiometria.

(iv) Mtoa huduma atatunza taarifa za Taasisi na za mwakilishi wa taasisi.

(v) Laini ya simu itakayosajiliwa itakuwa na jina la taasisi.

11. Utaratibu wa kusajili laini zinazotumiwa na walio kati ya miaka 12 na 18

i. Laini za simu zinazotumiwa na watoto zitasajiliwa chini ya kipengele cha usajili wa biometria wa watoto

ii. Mzazi/ mlezi atatakiwa kuwasilisha nakala iliyothibitishwa ya hati za uasili au cheti cha kuzaliwa na/au pasipoti yenye visa inayotumika, picha ya mototo na uraia wake.

iii. Mzazi/mlezi atawakilishi wa kampuni atawasiliaha kitambulisho chake cha NIDA na uhakiki wa alama za vidole mara moja kwa kadi zaidi ya moja anayosajili kibiometria

iv. Laini ya simu itakayosajiliwa itakuwa na jina la mtoto.

v. Baada ya kufikia umri wa miaka 18, mtoto atatakiwa kusajili upya laini husika aktumia kitambulisho chake cha NIDA.

vi. Watoa huduma watamtaarifu mototo mezi mitatu (3) kabla ya tarehe ya kufika miaka 18 na watampa miezi mitatu (3) ya kujiandaa ili kumwezesha motto kusajili upla yaioni yake.

vii. Pale ambapo mototo atashindwa kujitokeza kwa ajili ya kusajili upya laini ndani ya kioindi cha miezi mitatu baada ya kufikikia miaka 18, mtoa huduma ataizima laini husika kwenye mtandao wake.

12. Utaratibu wa kusajili laini kwa raia wa nje/wageni wanaoingia nchini

Laini za simu zinazotumiwa na raia wa nje/wageni wanaoingia nchini zitasajiliwa chini ya kipengele cha usaijili wa laini kibiometria wa raia wa nje/wageni wanaoingia nchini.

(i) Wageni watatakiwa kuwasilisha nakala ya pasipoti zenye VISA inayotumika na uhakiki wa alama za vidole kwa ajili ya usajili wa laini kibiometria.

(ii) Wageni wasiohitaji VISA kuingia nchini watatakuwa kuwasilisha nakala ya pasipoti na uhakiki wa alama za vidole kwa ajili ya usajili wa laini kibiometria.

(iii) Raia wa nchi nyingine watatakiwa kuwasilisha vitambulisho vya taifa na uhakiki wa alama za vidole kwa ajili ya usajili wa laini kibiometria.

(iv) Mtoa huduma atatunza taarifa za wageni au raia wa nje kama ipasavyo.

(v) Laini ya simu itakayosajiliwa itakuwa na jina la mgeni au raia wa nje anayehusika.

13. Utaratibu wa Kusajili Laini za Simu kwa Wakimbizi

(i) Laini za simu zinazotumiwa na wakimbizi zitasajiliwa chini ya kipengele cha usajili wa biometria kwa wakimbizi;

(ii) Mkimbizi atatakiwa kuwasilisha Kitambulisho chake ukimbizi/Namba ya kitambulisho cha ukimbizi kinachotolewa na NIDA na uhakiki wa alama za vidole kwa ajili ya usajili wa laini ya simu kibiometria utafanyika;

(iii) Mtoa huduma atahifadhi taarifa za mkimbizi kama kwenye kitambulisho chake; na

(iv) Laini ya simu itasajiliwa kwa jina la mkimbizi.

14. Utaratibu wa kusajili laini za simu kwa maafisa ubalozi/wana diplomasia

(i) Laini za simu zinazotumiwa na maafisa ubalozi/wana diplomasia zitasajiliwa chini ya kipengele cha usaijili wa laini wa maafisa ubalozi/wana diplomasia

(ii) Mwanadiplomasia atatakiwa kuwasilisha nakala ya pasipoti inayotumika na nakala ya kitambulisho cha kidiplomasia kutoka Wizara ya mambo ya Nje na Usirikiano Afrika Mashariki.

(iii) Alama za vidole hazitachukuliwa wakati wa usajili.

(iv) Mtoa huduma atatunza taarifa za mwanadiplomasia husika.

15. Utaratibu wa kusajili laini kwa taasisi za Kibalozi/Kidiplomasia

(i) Laini za simu zinazotumiwa na maafisa ubalozi/wana diplomasia zitasajiliwa chini ya kipengele cha usaijili wa laini wa taasisi za Kibalozi/Kidiplomasia

(ii) Taasisi za Kibalozi/Kidiplomasia zitatakiwa kuwasilisha barua ya utambulisho na barua kutoka Wizara ya mambo ya Nje na Usirikiano Afrika Mashariki.

(iii) Mwakilishi atatakiwa kuwasilisha pasipoti inayotumika na kitambulisho ha kidiplomasia kinachotumika kwa ajili ya kusajili laini zaidi ya moja kwa wakati mmoja.

(iv) Alama za vidole hazitachukuliwa wakati wa usajili.

(v) Mtoa huduma atatunza taarifa za mwanadiplomasia husika

(vi) Laini ya simu itakayosajiliwa itakuwa na jina la taasisi ya kibalozi/kidiplomasia.

16. Utaratibu wa kusajili katika hali ambapo majina hayafanani

(i) Pale ambapo majina ya mteja yanatofautiana na yale kwenye kitambulisho cha NIDA, mtoa huduma atatumia taarifa za matumizi; taarifa za kuongeza salio la muda wa maongezi, mawasiliano ya sauti, huduma za data na miamala ya pesa mtandao kuhakiki mmiliki ya laini

husika. Uhakiki huu utafanyika katika vituo vya huduma kwa wateja, maduka ya watoa huduma na ya wakala pekee.

(ii) Mtoa huduma atauliza maswali ya uhakiki wa matumizi kama ifuatavyo:

a) Taja namba **Tano** uloizopiga ndani ya siku 30 zilizopita.
b) Mara ya mwisho uliongeza salio la kiasi gani?
c) Kiasi gani cha data ulichonunua mara ya mwisho?
d) Ni kiasi gani cha muamala wa pesa mtandao mara ya mwisho?
e) Taja namba **Tano** ambazo unazofanyia miamala ya pesa mtandao mara kwa mara.

(iii) Baada ya kupata majibu sahihi ya maswali yote. Mteja atawasilisha alama za vidole kwa ajili ya uhakiki wa kibiometria.

(iv) Mtoa huduma atatuma taarifa ya mabadilio ya taarifa za usajili kwa njia ya ujumbe mfupi ndani ya saa 24 kwa ajili ya idhini ya mteja.

(v) Baada ya kupokea idhini ya mteja, mtoa huduma atafanya mabadiliko na kutunza kumbukumbu za NIDA na nyinginezo za awali.

(vi) Baada ya kubadilisha taarifa za usajili, huduma za pesa mtandao zinasitishwa kwa saa 24.

17. Utaratibu alama za vidole zisizoonekana au kwa wasio na vidole

a) Wateja ambao alama za vidole hazikuonekana au hawakuwa na vidole wakati wa Kujiandikisha NIDA

(i) Kwa wateja ambao hawana vidole au alama zao za vidole hazisomeki, na walipata vitambulisho vya NIDA wakiwa katika hali hiyo, watoa huduma watawasajili kwa kutumia Mfumo wa NIDA ambao utawauliza wateja maswali ambayo yanatokana na taarifa zao zilizopo NIDA.

(ii) NIDA itathibitisha kwamba mteja hana vidole au alama za vidole hazionekani.

(iii) Mteja atatakiwa kuwasilisha kitambulisho au Namba ya kitambulisho cha NIDA.

(iv) Mtoa huduma atauliza maswali kadhaa kuhakiki taarifa za mteja na atauliza maswali **matatu** yanayotokana na kanzidata ya NIDA.

(v) Baada ya kujibu kwa usahihi theluthi mbili (2/3) au asilimia 66 ya maswali, uhakiki utakuwa umekamilika.

(vi) Mtoa huduma atatunza taarifa zilizohakikiwa na NIDA.

(vii) Pale ambapo NIDA itaweka utaratibu mwingine wa kuhakiki, TCRA itatoa maelekezo kuhusu utaratibu wa kufanya uhakiki ipasavyo.

b) wateja ambao alama zao za vidole hazisomeki ama walipoteza vidole baada ya kupata namba ya kitambulisho cha taifa (NIN)

(i) Mtoa atampatia fomu mteja wake fomu maalum iliyoandaliwa na NIDA ili ajaze taarifa zake na kuiwasilisha hiyo fomu kwenye ofisi za NIDA zilizopo karibu.

(ii) NIDA atakamilisha utaratibu wa kuhakiki kuwa mwombaji hana vidole ama alama zake za vidole hazisomeki.

(iii) Baada ya siku mbili, mtoa huduma atamsajili mteja kwa kutumia Mfumo wa NIDA ambao utamuuliza mteja maswali ambayo yanatokana na taarifa zake zilizopo NIDA.

(iv) Mtoa huduma atatunza taarifa zilizohakikiwa na NIDA.

(v) Pale ambapo NIDA itaweka utaratibu mwingine wa kuhakiki, TCRA itatoa maelekezo kuhusu utaratibu wa kufanya uhakiki ipasavyo.

18. Usajili wa kibiometria katika mazingira maalum

(i) Pale ambapo mteja ametambulika kwamba anatoka kwenye taasisi ya serikali au wakala wa serikali aliyeidhinishwa na taasisi hiyo ya serikali na anataka kutokufanya uhakiki wa alama za vidole, mtoa huduma atamwelekeza mteja huyo kupata kibali cha TCRA kuhusu suala hilo.

(ii) Mteja ataiandikia TCRA kuomba kupata kibali cha kutokuhakiki kwa alama za vidole na katika maombi hayo ataelezea sababu za maombi yake.

(iii) Baada ya kupata kibali cha TCRA, mteja atarejea kwa mtoa huduma kwa ajili ya usajili wa laini.

(iv) Mtoa huduma atasajili laini kwa mujibu wa kibali cha TCRA, kwenye vituovya huduma kwa wateja, kwenye maduka ya mtoa huduma na ya wakala wa mtoa huduma.

SEHEMU YA IV
TOZO

19. Gharama na Tozo

Watoa huduma hawatawatoza wateja wao wakati wa usajili wa laini kibiometria.

SEHEMU YA V

MALALAMIKO YA WATEJA

20. Malalamiko ya Wateja

(i) Malalamiko yanayohsiana moja kwa moja na usajili wa laini kibiometria yataelekewa kwa watoa huduma za simu za mkononi, ambao watayashughulikia kupitia utaratibu wao wa kushughulikia malalamiko.

(ii) Iwapo malalamko hayatatatuliwa kati ya mteja na mto huduma za simu za mkononi, mteja ayawasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka ndani ya siku 14 za kazi kuanzia tarehe ambamo suala lake lilishindikana kutatuliwa ili liweze kushughulikiwa kwenye hatua za juu zaidi.

(iii) Malalamiko yanayopokelewa na Mamlaka yatawasilishwa kwa watoa huduma husika au NIDA pale inapofaa. Malalamiko ambayo hayahusiani na mtoa huduma moja kwa moja au NIDA, lakini yemetokana na usajili wa laini kibiometria, yatashughulikwa ma Mamlaka pale inapowezekana na/au inapofaa.

(iv) Katika hali ambapo malalamiko hayakutatuliwa kwa namna ya kumridhisha Mlalamikaji, ni majukumu ya mtoa huduma za simu za mkononi ambaye malakamiko yamewasilishwa kwake kumjulisha Mlalamikaji kuhusu haki zake ambazo anaweza kuzifuatilia kwenye ngazi za juu zaidi au rufaa.

SEHEMU YA VI

KUZUIA ULAGHAI

21. Kuzuia Ulaghai

(i) Watoa huduma wote wa huduma za simu za mkononi watakubaliana kushirikiana kwa nia njema kuzuia, pale inapowezekana, matukio ya ulaghai au shughuli ambazo hazikuidhinishwa kuhusiana na usajili wa laini kibiometria.

(ii) Iwapo matukio ya ulaghai yatabainika, watoa huduma za simu za mkononi watajitahidi kushirikana kutambua ulaghai huo na kuchukua hatua dhidi ya wahalifu wanaotenda ulaghai huo.

(iii) Shughuli zote za ushrikiano zitafanyika kwa mujibu wa sheria zilizopo za hifadhi ya data na faragha/usiri kulingana na hali iliyopo; na pia zitazingatia sheria zilizopo za makampuni au biashara ambazo zitafaa.

(iv) Mtoa huduma ambaye atashindwa kuwabaini wahalifu wanaofanya shughuli zozote ya ulaghai kuhusiana na usajili wa laini kibiometria atawajibika kumfidia mhanga wa matuko ya ulaghai kwa hasara watakayopata.

(v) Pale ambapo Kitambulisho cha Taifa kimethibitishwa kwamba kimehusika kwenye shughuli za ulaghai, taarifa za kitambulisho hicho cha Taifa zitawasilishwa NIDA ili kukizuia kisifanye shughuli za uhalifu kwa siku 90.